**PRIMARY EDUCATION SERVICES NETWORKING ORGANIZATION (PESNO)**

**SIMU: 0713- 526533**

**0767- 526533**

# MTIHANI WA PILI WA UTAMILIFU KWA DARASA LA SABA

# SOMO: MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI [06]

**TAREHE 04/05/2021 MUDA: SAA 1:30**

**JINA LA MTAHINIWA:** ______________________________________________

**JINA LA SHULE:** ________________________________________________________

**WILAYA**: _________________ **MKOA:** __________________

## MAELEKEZO:

1. Jaza nafasi wazi hapo juu na katika karatasi ya majibu
2. Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.
3. Chagua jibu sahihi kisha siliba herufi yake katika karatasi ya kujibia (OMR)kwa kutumia kalamu ya risasi kuanzia swali 1 hadi 40
4. Katika swali la 41 hadi 45 jibu maswali kwa kuandika majibu nyuma ya karatasi ya (OMR)
5. Hakikisha kazi yako iko nadhifu na safi
6. Mtihani huu una kurasa nne zilizochapishwa


**SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA**

**Chagua jibu sahihi kisha siliba herufi ya jibu hilo katika karatasi ya kujibia uliyopewa**

1. Jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka binadamu hujulikana kama:
   A. Uoto B. Angahewa C. Makazi D. Mazingira E. Milima
2. Ipi kati ya hizi zifuatazo ni njia sahihi zaidi ya kutunza mazingira dhidi ya takataka za viwandani?
   A. Urejeleaji wa takataka C. Kutupa takataka ovyo E. Kutumia bidhaa za asili
   B. Kutupa takataka mtoni au ziwani D. Kuchoma takataka
3. Watu wanaoishi katika maeneo yenye miinuko mikali wapo katika hatari ya kuathiriwa na janga lipi la asili kati ya haya yafuatayo?
   A. Ukame B. Mlipuko wa volkano C. Mafuriko D. Tsunami E. Maporomoko ya udongo
4. Binadamu alikula chakula kibichi katika zama zipi?
   A. Zama za Mawe za Kati C. Zama za Mawe za Mwisho E. Zama za Chuma
   B. Zama za Mawe za Kale D. Zama za Kidijitali
5. Mbali na kumbukumbu za nyaraka pamoja maktaba njia ipi kati ya hizi zifuatazo inaweza kutumika kuhifadhi taarifa za kihistoria katika kwa njia ya maandishi?
   A. Makumbusho B. Vifaa vya kieletroniki C. Anthropolojia D. Akiolojia E. Maeneo ya kihistoria
6. Ushonaji, uchoraji, upambaji, uchongaji na ufinyanzi ni mifano ya aina gani ya sanaa?
   A. Sanaa ghibu B. Sanaa za maigizo C. Sanaa za fasihi D. Sanaa za maonyesho E. Ufundi
7. Ili kuweza kukusanya matone ya maji ya mvua, kipima mvua yafaa kiwekwe umbali gani kutoka ardhini?
   A. Sentimeta 15 B. Sentimeta 30 C. Sentimeta 30 D. Sentimeta 100 E. Sentimeta 15
8. Ipi kati ya hizi zifuatazo ni njia sahihi ya kuzuia majanga ya moto?
   A. Kutumia vifaa bandia vya umeme D. Kuielimisha jamii namna ya kuzuia ajali za moto
   B. Kurina asali kwa kutumia moto E. Kuvuta sigara karibu na vituo vya mafuta
   C. Matumizi mabaya ya vifaa vya umeme
9. Mojawapo kati ya hizi SIYO faida itokanayo na upandaji wa miti:
   A. Miti hutupatia kivuli D. Husaidia kutokea kwa mvua
   B. Miti huongeza rutuba kwenye udongo E. Miti huzuia mmomonyoko wa udongo
   C. Miti hutupatia madini
10. Mabadiliko ya tabia ya nchi yana athari gani kwa wakulima na wafugaji?
    A. Kuyeyuka kwa barafu D. Mazao kukauka na mifugo kufa kwa ukame
    B. Kuongezeka kwa kina cha bahari E. Upatikanaji wa mvua
    C. Udongo kuwa na rutuba
11. Kazi kuu ya BAKITA ni nini?
    A. Kusimamia sanaa ya Tanzania D. Kuimarisha michezo nchini
    B. Kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili E. Kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi
    C. Kuhamasisha matumizi ya lugha za kigeni
12. Miongoni mwa njia za kutokomeza mila na desturi zilizopitwa na wakati nchini Tanzania ni:
    A. Kuiga utamaduni wa kigeni D. Kuielimisha jamii
    B. Kupunguza matumizi ya Kiswahili E. Kuendeleza mila na desturi potofu
    C. Kuhimiza ukeketaji wa wanawake
13. Sentensi ipi kati ya hizi zifuatazo inaonesha ushirikiano wa kiuchumi baina ya Tanzania na mataifa mengine?
    A. Kufungua balozi za Tanzania katika mataifa mengine
    B. Mataifa mengine kuwa na balozi zao nchini Tanzania
    C. Viongozi wa Tanzania kushiriki sherehe za kitaifa katika nchi nyingine
    D. Kushirikiana na nchi zingine katika shughuli za kibiashara, nishati na uchukuzi
    E. Viongozi wa nchi nyingine kuhudhuria shughuli za misiba ya viongozi wetu
14. Miongoni mwa sababu za kiuchumi zilizochangia muingiliano baina ya Pwani ya Afrika Mashariki na nchi za Kiarabu kuanzia karne ya nane ilikuwa:
    A. Kueneza dini ya Uislam C. Kueneza utamaduni wa Ulaya E. Kufanya biashara
    B. Kueneza dini ya Ukristo D. Kuanzisha ukoloni
15. Shujaa wa Afrika aliyepigana na Waingereza nchini Misri mnamo mwaka 1882 alikuwa nani?
    A. King Menelik II C.Urabi Pasha E. Ahmed Sekou Toure
    B. King Pharaoh D. Sir. Abubakar Tafawa Balewa

16. Utawala wa Waingereza nchini Zanzibar ulifika kikomo mnamo mwaka gani?
A. 1913 B. 1890 C. 1963 D. 1964 E. 1961
17. Taifa lipi la Ulaya lilitawala Rwanda na Burundi baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia?
A. Ujerumani B. Ureno C. Uingereza D. Italia E. Ubelgiji
18. Ni mfumo upi wa utawala ulitumiwa na Waingereza kwa mara ya kwanza huko Nigeria Kaskazini?
A. Utawala wa moja kwa moja C. Utawala wa ushirikiano E. Ubaguzi wa rangi
B. Utawala wa mlango wa nyuma D. Utawala wa kulisha kasumba
19. Nchi nyingi za Afrika zilipata uhuru wao katika miaka ya:
A. 1950 B. 1970 C. 1960 D. 2000 E. 1900
20. Gavana wa mwisho wa Waingereza nchini Tanganyika alikuwa nani?
A. Horace Byatt C. Donald Cameron E. Julius Von Soden
B. Richard Turnbull D. Edward Twinning
21. Tukio lipi kati ya haya yafuatayo liliathiri kwa kiasi kikubwa awamu ya pili ya maendeleo ya kiuchumi nchini Tanzania kati ya mwaka 1967 na 1985?
A. Mfumo wa chama kimoja D. Kujiuzuru kwa mwl. J. Nyerere katika kiti cha Urais
B. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar E. Kutangazwa kwa Azimio la Arusha
C. Vita vya Kagera
22. Mimi siyo nyota wala siyo sayari. Ni satelaiti asilia. Sina mwanga wa asili isipokuwa naakisi mwanga kutoka kwenye jua na kuimulikia dunia wakati wa usiku. Je, mimi ni nani?
A. Jua B. Mwezi C. Nyota D. Asteroidi E. Kimondo

**Chunguza kwa makini ramani ifuatayo kisha jibu swali la 23, 24 na 25**




23. Aina ya uoto inayoonyeshwa kwa herufi **A** inaitwaje?
A. Montane vegetation C. Uoto wa mikoko E. Uoto wa kisavana
B. Uoto wa kitropiki D. Uoto wa miyombo
24. Herufi gani inawakilisha uoto wa miyombo?
A. C B. A C. B D. E E. D
25. Ipi kati ya hizi zifuatazo ni sifa ya uoto wa asili unaoonyeshwa kw a herufi **D**?
A. Miti iliyotawanyika na vichaka C. Mountain forests E. Mimea aina ya mikaratusi
B. Misitu minene, miti mirefu na vichaka D. Vichaka, miti mirefu na nyasi ndefu
26. Mwalimu wa somo la Maarifa ya Jamii aliwaambia wanafunzi wa darasa la saba wachore ramani ya bara la Afrika. Je, ni aina gani ya kipimio cha ramani ingefaa kwa ramani hiyo?
A. Kipimio cha mstari C. Kipimio kidogo E. Kipimio kikubwa
B. Kipimio cha sentensi D. Kipimio cha kati
27. Mstari wa latitudo wenye nyuzi $66\frac{1}{2}^{0}$ Kusini mwa Ikweta unaitwaje?
A. Ikweta C. Tropiki ya Kansa E. Mzingo wa Aktiki
B. Meridiani Kuu D. Mzingo wa Antaktiki
28. Ipi kati ya hizi zifuatazo ni orodha sahihi ya rasilimali asilia zilizopo Tanzania?
A. Ardhi, maji na madini D. Misitu, reli na maji
B. Madini, maji na miundombinu E. Barabara, reli na viwanja vya ndege
C. Milima, mabonde na barabara
29. Madini yapi huchimbwa mkoani Manyara ambayo huiingizia Tanzania fedha za kigeni?
A. Shaba B. Ulanga C. Dhahabu D. Chuma E. Tanzanaiti

30. Sensa ya watu na makazi nchini Tanzania hufanyika kila baada ya miaka mingapi?
   A. Mitano B. Kumi C. Kumi na mbili D. Kumi na tano E. Ishirini
31. Kitendo cha mtu kutoka nchi moja kwenda kuanzisha makazi ya kudumu katika nchi nyingine hujulikana kama:
   A. Mkimbizi B. Uharamia C. Uhamiaji E. Uhamaji E. Makazi
32. Zifuatazo ni sababu za kijiografia ambazo huathiri mtawanyiko wa watu katika eneo husika, ISIPOKUWA:
   A. Aina ya udongo B. Tabia ya Nchi C. Huduma za Kijamii D. Sura ya Nchi E. Uoto
33. Aina ya ufugaji ambapo wafugaji hufuga kwa kuhama hama kutoka eneo moja hadi nyingine kutafuta malisho hujulikana kama:
   A. Ufugaji wa mifugo mingi C. Ufugaji wa zizini E. Ufugaji wa ranchi
   B. Kilimo cha kuhamahama D. Ufugaji wa kuhamahama
34. Njia za kilimo zisizofaa zina athari gani kwa mazingira?
   A. Kuhifadhi mazingira C. Huleta mavuno mengi E. Upotevu wa madini
   B. Huharibu udongo D. Husaidia kuhifadhi udongo
35. Ni zao lipi kati ya mazao yafuatayo hutumika kama malighafi ya kutengenezea sigara?
   A. Kahawa B. Kakao C. Pamba D. Tumbaku E. Pareto
36. Chombo cha serikali chenye mamlaka ya kudhibiti ubora wa bidhaa za wajasiriamali nchini Tanzania hujulikana kama:
   A. TMAA B. TRA C. TBC D. TCRA E. TBS
37. Benki ni taasisi muhimu kwa mjasiriamali kwa sababu:
   A. Hutoa mikopo na ushauri juu ya uendeshaji wa biashara D. Humuandalia mjasiriamali kitabu cha mauzo
   B.Humsaidi mjasiriamali kuendesha biashara yake E. Humsaidia mjasiriamali kutafuta wateja
   C. Hutoza kiasi kikubwa cha riba na hivyo kuongeza uzalishaji
38. Wakati sahihi wa kuosha mikono kwa maji safi na sabuni ni upi?
   A. Kabla na baada ya chakula C. Kabla ya chakula E. Kabla ya kulala
   B. Muda wote wakati wa chakula D. Baada ya chakula
39. Filimbi, tarumbeta na zumali ni mifano ya:
   A. Ala za muziki za kiasili
   B. Ala za muziki za kisasa
   C. Ala za muziki zinazotoa sauti za kuimbika
   D. Ala za muziki zinazotoa sauti zisizoimbika
   E. Ala za muziki zinaotoa sauti kwa kutikiswa
40. Miongoni mwa madhara ya kushindwa kufuata misingi na kanuni za chakula ni pamoja na:
   A. Kuimarisha usafi wa chakula C. Kulala E.Kuvimbiwa
   B. Kuwa na afya bora D. Ulafi

**SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI**

**Jibu swali la 41-45 kwa kuandika majibu sahihi katika karatasi ya kujibia uliyopewa**

41. Kwanini wanawake wanashauriwa kuzingatia kanuni za usafi pindi wanapokuwa kwenye hedhi?
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
42. Ni kwa namna gani matumizi ya nishati mbadala hupunguza kiwango cha uchafuzi wa mazingira?
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
43. Kwanini mkutano wa kuligawa bara la Afrika miongoni mwa mataifa ya Ulaya ulioitishwa na Kansela wa Ujerumani Otto Von Bismarck uliitwa Mkutano wa Berlin?
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
44. Tafuta longitudo ya mji **Q** ambapo ni saa 9:00 mchana ikiwa ni saa 7:00 mchana katika mji **P** uliopo longitude nyuzi $15^{o}$ Mashariki
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
45. Elezea kwa kifupi ni kwa jinsi gani shughuli za uchukuzi zimechangia kuimarisha ushirikiano baina ya Tanzania na nchi za jirani.
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________